SALAMU ZA MKUU WA MKOA WA RUKWA NDUGU ZELOTE STEPHEN ZELOTE KATIKA MAADHIMISHO YA SHEREHE YA WAFANYAKAZI MEI MOSI MWAKA 2017 ZILIZOFANYIKA KIMKOA WILAYA YA NKASI TAREHE 01 MEI, 2017

Ndugu Mwenyekiti wa TUCTA,

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa,

Wakurugenzi wa Halmashauri zote,

Makatibu wa Vyama vya Wafanyakazi,

Viongozi wa vyama vingine vya siasa,

Ndugu wafanyakazi wote mliopo hapa na hasa wale ambao walitarajia kushiriki lakini wakashindwa kwasababu zilizo nje ya uwezo wao,

Wana habari wa Redio, Televisheni na Magazeti.

Ndugu Mwenyekiti

Imenipasa kutumia nafasi hii na ama sisi wote kwa ujumla kumshukuru mola wetu kwa kutupa uzima na kutuwezesha kufika katika eneo hili kwa ajili ya sherehe hizi za wafanyakazi ya Mei Mosi. Ni vyema wote tukamwambia Mungu Asante na kumuomba aendelee kutulinda na abariki Taifa letu na Amani yetu chini ya Rais DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI mchapakazi namba moja kwa kiwango cha juu mno.

Ndugu Mwenyekiti

Imenipasa vile vile kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu nyingi na za dhati kwako na wengine wote katika Mkoa wa Rukwa kwa Mualiko huu kuja kuwa mgeni rasmi lakini pia nataka nikwambie ukubali kuwa nami nimekuja kwasababu ni mfanyakazi. Na hivi hapa sasa pia niko kazini.

Ndugu Mwenyekiti

Kadhalika inanipasa nitumie nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wote katika Mkoa wa

Rukwa haswa wale wote ambao kwa kipindi chote wamefanya kazi kwa uadilifu, nidhamu na uzalendo na kuleta mafanikio chanya kwa manufaa na maslahi ya Mkoa wetu na Taifa Letu kwa Ujumla, jambo hili nalisema kwa wote waliopo Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Sekta ya Umma, binafsi na nyinginezo. Nawapongeza wote wanaokwenda sambamba na kauli mbiu ya Rais wetu “HAPA KAZI TU”. Wote nawapa “Big – up”.

Ndugu Mwenyekiti

Mafanikio ya wafanyakazi yakiwepo ni ishara njema kwamba TUCTA katika Mkoa wa Rukwa chini ya uwenyekiti wako inawalea na kuwahudumia vyema wafanyakazi kwa kuzingatia mfumo wa taratibu, kanuni na sheria zinazotawala ajira.

Ndugu Mwenyekiti

Nikupongeze na wote mnaounda uongozi wa TUCTA kuanzia sehemu za kazi hadi ngazi ya Mkoa. Nipende pia kuwashukuru kwa namna ambavyo mnaonyesha ushirikiano kwa serikali.

Ndugu Mwenyekiti

Shukrani zipo nyingi; Nimevutiwa sana kwa utaratibu huu mliojiwekea kwa sherehe hii kufanyika kwa mzunguko kila Wilaya. Mwaka jana nakumbuka zilifanyika katika Wilaya ya Kalambo. Na sasa mwaka huu hapa Nkasi. Nawapongeza sana. Najua mnafuata nyayo za Mheshimiwa Rais wetu DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI. Sherehe zinazoadhimishwa Kilimanjaro na yeye akiwa mgeni rasmi. Utaratibu huu ni mzuri na niwatake hata wengine waige badala ya kila jambo kuwa la sehemu moja. Hata mechi za mpira zinazopangwa kwenye maeneo tofauti. SOLIDARITY, SOLIDARITY, SOLIDARITY.

Ndugu Mwenyekiti

Wakati naingia katika Mkoa huu niliwataka watumishi wote katika sehemu za kazi wazingatie yafuatayo:-

1. Team work spirit.
2. Field work.
3. Hard work.
4. Good work.

Lakini pia niliahidi kulala kwa saa nne na nyingine zote ni “kazi tu”. Narudia tena leo kusisitiza maagizo hayo na msimamo wangu. Naamini Ndugu Mwenyekiti wa TUCTA itaondoka pia na hayo.

Ndugu Mwenyekiti,

Leo ni maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi kote Duniani yenye Kauli Mbiu:

“UCHUMI WA VIWANDA UZINGATIE KULINDA HAKI, MASLAHI NA HESHIMA YA MFANYAKAZI”

Jambo kubwa mbalo naamini kila Mtanzania analifurahia na kutaka litimie ni Rais wetu DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI la kujenga uchumi wetu kwa kujenga viwanda. Tunahitaji viwanda katika Mkoa wetu. Mkoa wa Rukwa una mazao ya kutosha ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Madini. Ili kupiga hatua kuongeza pato la kila mwananchi, tunahitaji viwanda kwaajili ya kuongeza thamani ya mazao yetu. Pengine tunapozungumza viwanda watu wanawaza

majengo makubwa na mitambo mikubwa, La hasha. Tuanze na viwanda vidogo.

Ndugu Mwenyekiti

Nitoe mfano mdogo, wafugaji wa kuku hawapati chakula cha kutosha. Mkoa wa Rukwa kwa kiwango kikubwa una mahitaji yote ya kutengeneza chakula cha kuku, lakini hatuna kiwanda hicho. Tunauza mazao yetu bila ya kuongeza thamani ili kwenda kunufaika sehemu zingine na inarudi kwetu na kununua ghali.

Kwenye duka la viatu tukihitaji kununua tunauliza ngozi halisi (pure leather). Ngozi halisi inatoka Rukwa kwanini tusiwe na viwanda vya kusindika ngozi badala ya kuwaachia watu wa nje kuja kukusanya ngozi zetu kwa bei ya kutupa halafu ikirudi imeongezwa thamani tunanunua ghali. Tunasikia wenzetu humu nchini wanaolima pamba wanasema sasa basi pamba hata zinazohitajika, mahospitalini itengenezwe nao wenyewe**.** Vipo Rukwa, mahindi, ngano, maharage, soya, maziwa, nyama, ngozi, alizeti, ufuta, ulezi, mbaazi, mpunga, samaki, dagaa.

Ndugu Mwenyekiti

Nataka niwape uhakika ufuatao:-

Tukifanikiwa kwenye suala la kuanzisha viwanda vyetu wenyewe ninaamini suala la kuzingatia, kulinda haki, Maslahi na heshima ya mfanyakazi halitasumbua serikali na hasa hii inayoongozwa na DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI ambaye katika kila sentensi yake haachi kutaja wanyonge au wananchi wa kawaida. Serikali itafarijika zaidi endapo TUCTA itaungana na juhudi za serikali kuhamasisha ujenzi wa viwanda ili na ajira ziongezeke ndipo ifuate na mambo mengine kama ilivyo katika kanuni, taratibu na sheria na ile mikataba ya Kimataifa ILO.

Ndugu Mwenyekiti

Nashukuru sana kwa risala yenu ambayo mmeonesha imegawanyika katika sehemu tatu, kwamba yapo yale ya kitaifa, na mimi kwa kweli sitegemei kuyagusa zaidi ya kusema tutayaelekeza kwenye ngazi hiyo. Mengine ni ya waajiri na yale yaliopo kwenye ngazi yangu.

Ndugu Mwenyekiti

Najua mlikuwa mnanisikiliza lakini niwaombe mtege masikio kwa haya machache nitakayosema:-

1. Tuendelee kumuunga Mkono sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua mbalimbali anazochukuwa kuleta maendeleo katika nchi yetu na kuboresha maisha ya watanzania wakiwemo na wafanyakazi.
2. Sehemu ya uchumi wetu ni viwanda na kuongeza thamani bidhaa zetu.
3. TUCTA iendelee kusaidiana na Serikalikujenga uwadilifu, uwajibikaji, uzalendo na nidhamu kwa wafanyakazi wote.

Ndugu Mwenyekiti

Sote tunafahamu kwamba Serikali ya awamu ya tano dhamira yake ni pamoja na kulinda maslahi ya watumishi wote. Katika changamoo mlizotaja kwenye risala ni pamoja na la watumishi waliopandishwa madaraja kutolipwa mishahara kulingana na madaraja yao na hasa wengine kufutiwa vyeo vipya walivyopewa. Ni vyema

wote tukafahamu kwamba Serikali ilisimamia kuimarisha mambo mbalimbali katika utumishi ili kuondoa kasoro zilizokuwepo kwenye ajira likiwepo la watumishi hewa, makato hewa, likizo hewa, matibabu hewa, vyeti feki, uhamisho hewa**.** Katika hali hiyo mambo mazuri yasingewezekana. Huwezi ukapakuwa chakula na kuweka kwenye sahani chafu lazima uisafishe kwanza.

Ndugu Mwenyekiti

Katika Mkoa wa Rukwa Peke yake tulikuwa na watumishi hewa 647, vyeti feki 154. Pengine hata watumishi wanaodai wamepandishwa madaraja na hawalipwi mishahara ya madaraja ni hao hewa.

Waajiri hawataki kufanyika mabaraza ya wafanyakazi.

- Naagiza waajiri wote kuanzia sasa wahakikishe mabaraza ya wafanyakazi yanafanyika kwa taratibu zilizopo sehemu za Kazi.

Wafanyakazi bora kutolipwa tangu wachaguliwe mwaka 2015

- Endapo wapo watumishi bora ambao hawajalipwa nataka nipate majina yao mara moja, vinginevyo ifikapo tarehe 15 Mei, 2017 wawe wamelipwa.

Kupatikana wafanyakazi bora naagiza waajiri TUCTA washirikishwe.

Nyumba za waalimu

- Mahitaji ni Mkubwa. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 zimejengwa nyumba 1824 waalimu wa shule ya msingi.
- Sekondari 314
- Juhudi za ujenzi wa nyumba za watumishi unaendelea Kalambo.

Watumishi wanadai madai yao

- Mwaka 2015/2016 kiasi cha Sh.438, 767,730 kulifanikiwa kulipa madeni ya watumishi kwa mchanganuo ufuatao:-

    1. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo Tshs. 108,790,310

2. Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga Tshs. 126,837,040
3. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Tshs. 17,800,600
4. Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi Tshs. 55,365,500
5. Sekretarieti ya Mkoa Tshs. 129,974,280

- Agizo langu kwa sehemu zote hizo nilizotaja kuanzia sasa wawe makini kuepusha kuiingiza Serikali katika kuzalisha madeni yasiokuwa ya lazima.

- Ni vyema pia kufahamu kwamba baadhi ya madeni ya zamani yamelazimika kufanyiwa uhakiki kutokana na wimbi kubwa la udanyanyifu a madeni hewa pamoja na kukosekana nyaraka muhimu.

Waajiri kutopeleka michango ya akiba kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

- Utaratibu huu ni wa kisheria, nataka nipate taarifa ya kina kuhusu madai haya na ikibainika

wapo waajiri wanaokiuka utaratibukisheria lazima zichukuliwe mara moja.

Mfanyakazi anayestaafu kuhangaika kufuatilia mafao

- Napenda kuwashauri wale wanaotegemea kustaafu watoe taarifa mapema na kuambatanisha nyaraka zinazohusika
- Waajiri kupitia mapato yao ya ndani wahakikishe wanawasafirisha wastaafu na mizigo yao mara wanapostaafu**.**

Hata hivyo yanapotokea matatizo ya kuzungushwa taarifa ziletwe kwangu mara moja ili hatua zinazostahili zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kushughulika na mwajiri mzembe

Ndugu Mwenyekiti

Napenda nimalizie kwa kuwatakia wafanyakazi wote kila la kherikatika maadhimisho ya siku ya Mei Mosi kwamba ni mwanzo mwingine wa kupiga hatua ya maendeleo katika Mkoa wetu na Taifa letu.

SOLIDARITY, SOLIDARITY, SOLIDARITY.